

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA**



**TANGAZO LA AJIRA**

Jeshi la Polisi Tanzania linatangaza nafasi za ajira kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa vijana waliopo kwenye kambi za JKT/JKU ambao wamemaliza mafunzo ya awali katika Operesheni Kikwete na Operesheni Magufuli wenye elimu ya Kidato cha Nne, Sita, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu na Shahada.


Waombaji watatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

1. Awe katika kambi za JKT/JKU na amemaliza mafunzo ya awali ya JKT/JKU katika Opereshemi zilizotajwa hapo juu.
2. Awe Mtanzania kwa kuzaliwa.
3. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 25 kwa wenye elimu ya Kidato cha Nne, Sita, Astashahada na Stashahada.
4. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 28 kwa wenye elimu ya Stashada ya Juu na Shahada.
5. Awe na elimu ya Kidato cha Nne aliyemaliza mwaka 2014, 2015, 2016 na 2017 mwenye ufaulu ufuatao;
  - Aliyemaliza mwaka 2014 awe na ufaulu wa GPA usiopungua 0.6
  - Aliyemaliza 2015, 2016 na 2017 awe na ufaulu usiozidi alama (Points) 30.
6. Awe na elimu ya Kidato cha Sita aliyemaliza mwaka 2014, 2015, 2016, na 2017 na kufaulu.
7. Awe na Astashahada au Stashahada aliyehitimu mwaka 2014, 2015, 2016 na 2017.
8. Awe na shahada aliyehitimu mwaka 2014, 2015, 2016 na 2017.
9.
  - Awe na cheti halisi cha kuzaliwa, vyeti vyaa taaluma (Academic certificates) pamoja na vyeti vyaa kuhitimu elimu aliyonayo (leaving certificate/transcript).

- Awe na picha 3 za rangi (passport size).
10. Awe na tabia njema iliyothibitishwa na Mkuu wa Kambi ya JKT/JKU.
  11. Asiwe na kumbukumbu za uhalifu.
  12. Awe na afya njema (kimwili na kiakili) iliyothibitishwa na Daktari wa Serikali.
  13. Awe hajaoa/hajaolewa au kuwa na mtoto
  14. Asiwe na alama za kuchora mwilini (Tattoo).
  15. Awe tayari kufanya kazi za Polisi mahali popote Tanzania.
  16. Awe na urefu usiopungua futi tano inchi tano (5.5') kwa wanaume na futi tano na inchi tatu (5.3') kwa wanawake.
  17. Waombaji watakaofaulu usaili ndio watakaochaguliwa.
  18. Awe hajawahi kutumia dawa za kulevya.
  19. Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya Polisi.
  20. Awe hajaajiriwa na Taasisi nyingine.
  21. Waombaji wote waandike barua za maombi wao wenyewe kwa mkono (hand written) wakiambatanisha nakala za vyeti kwa anuani ifuatayo;
- Inspeksa Jenerali wa Polisi,  
Makao Makuu ya Polisi,  
S.L.P 9141**
- Dar es salaam.**
- Barua za maombi ziwasilishwe kwa Mkuu wa Kambi ambae atazipeleka kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa husika kwa hatua zaidi.
22. Waombaji wenyе masomo/taaluma za Sayansi na Ufundu watapewa kipaumbele.
  23. Usaili utafanyika kwenye kambi za JKT/JKU alipo muombaji.
  24. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10/05/2018**.

Kwa maelezo/ufafanuzi zaidi kuhusu nafasi, sifa na vigezo pamoja na tarehe ya kuanza usaili tembelea tovuti ya Polisi kwa anuani ifuatayo:-  
[www.policeforce.go.tz](http://www.policeforce.go.tz)

Imetolewa na;

  
.....  
Albert M. Nyamhangwa – CP, ndc  
Kamishna wa Polisi - Fedha, Utawala na Lojistiki  
Makao Makuu ya Polisi  
S. L. P. 9141  
DAR - ES SALAAM.